*Shairi hili limetungwa na LG Fumbuka kufuatia mjadala uliokuwa ukiendelea katika Tanzanet kuhusu sera za Rais Benjamin Mkapa.*

# MBELE KAKIRI MAKOSA

1. Wasalaam waungwana, hodi hodi tanzanet,
   Kigogo tumembana, sasa yuko hatihati,
   CCM kaiona, kumbe ina mikakati,
   Mbele kakiri makosa, kumbe Mkapa kafuzu.

2. Anadai wapinzani, wake wamo kwenye neti,
   Omongoreme ni nani? Tuweni wakweli ati,
   Sisi tulishabaini, sasa kapigwa manati,
   Kumbe Mkapa kafuzu, Meya kakiri makosa.

3. Tuhuma zake Yozef, Mkapa kaegemea,
   Lakini kwa uzoefu, hapa kwetu Tanzania,
   Kwataka uangalifu, si vyema kuparamia,
   Bwana Mbele umekiri, kumbe Mkapa kafuzu.

4. Egemea CCM? Egemea serkali?
   Tumwulize Kulthumu, kama hii si halali,
   Chama chetu kulaumu, kwani wewe ni dalali?
   Purofesa yu chini pu! kumbe Mkapa kafuzu.

5. Kumbe Mkapa kafuzu, Dr Mbele kakiri,
   Yalimshinda Kamuzu, CCM ni mahiri,
   Toka Mbinga hadi Zuzu, tuimbeni mashairi,
   Meya Mbele umekiri? Kijasho kinakutoka..

6. Tamati nimalizie, na wala siendelei,
   Deadwood kina nyie, why cannot you see?
   Viva tout le Tanzanie, Monsieur Purofesa Mbelee,
   The mayor has eaten his words!!

*LGFumbuka (LGF),*
*Dar es Salaam.*
*31 Januari 2002*